



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO



Kumb Na.: BG/A/I.VOL.V/11

Tarehe: 01 Septemba, 2021

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MUDA WA MIEZI MITATU KWA KAZI YA  
MTEKNOLOJIA - RADIOLOJIA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo anatangaza nafasi ya kazi kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa kujaza nafasi ifuatayo; ambayo ni Ajira vya Mkatiba kwa fani ya Mionzi.

**1. Mteknolojia Daraja la II - Radiolojia (Nafasi 1)**

**a) Sifa ya Mwombaji**

- Awe amehitimu kidato cha Nne au Sita.
- Awe amepata Stashahada mafunzo (NTA LEVEL 5) katika fani ya Radiolojia katika chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**b) Kazi na majukumu ya Mtaalam wa Mionzi**

**Radiolojia atatekeleza majukumu yafuatayo;-**

- i. Kuwapima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lake la kazi
- ii. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi
- iii. Kukagua picha za X Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (Diagnostic Quality)
- iv. Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliotuma wagonjwa
- v. Kusimamia watumishi walio chini yake
- vi. Kutoa ushauri kuhusu masuala ya kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.
- vii. Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization)
- viii. Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.
- ix. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

*Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)*

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, Halmashauri ya Wilaya Bagamoyo, S.L.P. 59, BAGAMOYO Mkoa wa Pwani.

Simu Na: 023 2440164, Nukushi: 023 2440338 Barua Pepe: [ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz). Tovuti: [www.bagamovodc.go.tz](http://www.bagamovodc.go.tz)

c) Ngazi ya Mshahara

- Mwombaji atakayefanikiwa kuajiriwa kwa Cheo cha Mteknolojia wa Mionzi Daraja la II atalipwa mshahara wa TGHS B kwa mwezi.

2. MASHARTI YA JUMLA

- Barua ya maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA) vilivyothibitishwa na Wakili au Mahakama.
- Mwombaji aambatanishe picha mbili za rangi (Passport size) za hivi karibuni.
- Kwa wale waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe kwamba vyeti vyao vimehakikiwa na kuthibitishwa na mamlaka (TCU au NECTA) kulingana na ngazi ya Cheti.
- Maombi yaambatanishwe na maelezo binafsi (CV)
- Mwombaji awe na umri wa miaka 18 – 45

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia barua pepe "[ded.bagamoyo@pwani.go.tz](mailto:ded.bagamoyo@pwani.go.tz)". kwa anuani ifuatayo;

"Mkurugenzi Mtendaji,"  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P. 59,  
**BAGAMOYO.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **07 Septemba, 2021** saa **9:30 Alasiri**.

**NB: Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri [www.bagamoyodc.go.tz](http://www.bagamoyodc.go.tz)**

Limetolewa na;



Shauri Seleha

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA  
BAGAMOYO**